**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA WAKATI WA KUFUNGUA KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA UKUMBI WA TAKWIMU JIJINI DODOMA MNAMO TAREHE 18 APRILI, 2023**

---

- **Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi – Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa, Naibu Mwanasheri Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma;**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Wanahabari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

***NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.***

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii katika kikao hiki muhimu cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, nashukuru uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi na kufungua kikao hiki muhimu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali chini ya uongozi wako Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza majukumu mliyopewa kitaifa kwa ufanisi mkubwa.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Napenda pia kuwapongeza viongozi na wajumbe wote wa Baraza la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutimiza wajibu wenu wa kuwawakilisha watumishi wenzenu katika Baraza hili na kutenga muda ili kuhudhuria kikao hiki ikiwa ni utekelezaji wa **Tamko Na. 1 la mwaka 1970** na Sheria za kazi kama ilivyoelezwa na Mwenyekiti wa Baraza katika Hotuba yake.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Nimejulishwa kwamba dhumuni kuu la kikao hiki cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni **kupokea na kujadili Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.**

Natumaini wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mtakuwa makini katika kujadili na kuchambua vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kuhakikisha mafanikio mliyofikia mwaka wa fedha 2022/2023 yanazidi kuongezeka.

Nawasihi wajumbe wote wa Baraza la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mzingatie mada na masuala yote yatakayowasilishwa na ambayo yameshawasilishwa katika kikao hiki katika kuboresha utendaji katika maeneo yenu ya kazi na mzidi kuwa wabunifu ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo na zitakazoibuliwa na watumishi kwa kuzingatia maslahi na ustawi, uwajibikaji na ufanisi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Taasisi inayojitegemea ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mujibu wa Kanuni Na. B.2 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la 2009. Ofisi imeanzishwa chini ya Ibara ya 59(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268.

Jukumu la msingi la Ofisi hii ni kuishauri Serikali kuhusu mambo yote ya kisheria kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanasimamiwa na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 na Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Kwa mujibu wa Hati Rasmi ya Rais ya Maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 2018, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina majukumu yafuatayo:-

a) Kuishauri Serikali katika masuala ya Mikataba na Uandishi wa Sheria;

b) Kuratibu na kutoa ushauri wa kisheria;

c) Kuendesha majadiliano kwa niaba ya Serikali katika mikataba yote;
d) Kuandaa miswada ya sheria kwa ajili ya kupitishwa na Bunge;
e) Kupitia mikataba ya kibiashara na ya kimataifa kwa niaba ya Serikali na kuishauri Serikali ipasavyo;
f) Kutoa miongozo ya kiutendaji;
g) Kusimamia na kuongoza vikao vya Timu ya Serikali ya Masuala ya Sheria (Government Legal Team);
h) Kusimamia wajibu wa kimikataba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
i) Kuandaa hati zote za kisheria na maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge;
j) Kushauri Wizara, Idara za Serikali na taasisi nyingine za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusiana na mchakato wa kutunga sheria;
k) Kushiriki katika kudhibiti nidhamu ya Mawakili wa Kujitegemea kupitia Kamati ya Maadili ya Mawakili (Advocates Committee);
l) Kuendesha na kusimamia mafunzo kwa njia ya vitendo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo;

m) Kuwasimamia Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wote walioko katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kutekeleza majukumu yao ya kisheria;

n) Kushauri kuhusu Sera za Nchi kuhusiana na usimamizi na utawala wa Sheria Tanzania pamoja na kusimamia taalum ya Sheria;

o) Kutoa ushauri kuhusiana na Nyaraka za Baraza la Mawaziri kama vile *cabinet papers* na memorandamu na ufuatiliaji wa ahadi za utekelezaji wa maamuzi yanayohitaji kutungwa kwa Sheria ama kuundwa chombo chochote cha kisheria; na

p) Kutekeleza jukumu lolote linaloweza kuwa muhimu kwa utekelezaji ulio na ufanisi wa majukumu na utekelezaji wa mamlaka ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Naomba mtambue kuwa, Baraza hili lina wajibu wa kuhakikisha majukumu niliyoyataja yanatekelezwa kikamilifu kwa kuzingatia matakwa ya Katiba, Sheria Kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali. Hivyo, nichukue fursa hii kuwakumbusha wajumbe wa Baraza hili kuendelea kutekeleza majukumu yenu kwa weledi na uadilifu kwa kuzingata maslahi mapana ya Serikali na Taifa kwa ujumla.

Aidha, uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali una wajibu wa kuhakikisha kila mtumishi anatekeleza wajibu wake na kuhakikisha hatua za kinidhamu zinachukuliwa dhidi ya watumishi ambao hawatekeleza wajibu wao.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Nafahamu kwamba mnazo changamoto nyingi ikiwemo upungufu wa vitendea kazi na watumishi, ufinyu wa bajeti, viwango vidogo vya mishahara na maslahi ya watumishi ambavyo havikidhi mahitaji halisi ya maisha na uendeshaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, nimebaini kuwa idadi ya watumishi na vitendea kazi bado haijitoshelezi licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kuimarisha mifumo ya kufuatilia utendaji kazi na kudumisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi, ujenzi wa Vituo Jumuishi, kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kurahisiha na kuharakisha utendaji kazi, kutoa mapendekezo ya kuboresha maslahi ya watumishi, kuongeza idadi ya watumishi na kuwapata watumishi vitendea kazi licha ya changamoto zilizopo.

Ni ukweli usiopingika kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamedhihirisha sifa za uongozi na za kiutendaji ndio maana wamepewa dhamana kubwa ya kuongoza na kusimamia Ofisi hii ambayo ina changamoto mbalimbali ili waweze kukabiliana nazo. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya na tunatumaini kuwa mtaendelea kufanya vizuri zaidi ya hapo.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Kwa kuwa nimefahamishwa kuwa kikao hiki cha Baraza kitafanyika kwa siku moja na hivyo kuna mambo mengi ya kujadili, naomba mniruhusu niweze kutumia muda mfupi kutoa maoni na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

(a) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wote kwa ujumla waendelee kulitumia Baraza la Wafanyakazi ili kujadili changamoto mbalimbali za watumishi na kushauri namna bora ya kutatua changamoto hizo;

(b) Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi, menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wahakikishe wanatekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa

kuendelea kufanya tathmini ya utendaji kazi, kufuatilia utekelezaji wa mikataba ambayo Serikali ina maslahi, kutumia kwa uangalifu vifaa vya TEHAMA na kudumisha umoja na ushirikiano uliopo baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi nyingine.

(c) Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kukamilisha ujenzi wa vituo jumuishi katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Tanga, Mtwara na Kilimanjaro.

(d) Nawasihi Mawakili wote wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali waendelee kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuendesha na kusimamia mashauri ya madai na jinai kwa niaba ya Serikali kwa kuzingatia maslahi ya Serikali na nchi kwa ujumla.

(e) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iendelee kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 na Mpango Mkakati wa mwaka (2021/2022 - 2025/2026) hususan katika kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kuimarisha uhamasishaji wa

rasilimali, usimamiaji na uwajibikaji na kuongeza ujuzi na uelewa wa umma kwenye masuala ya sheria;

(f) Napenda kuwahimiza kwa umoja wenu, mjenge Utumishi wa Umma wenye kuzingatia Kanuni za maadili ya Utumishi zilizopo pamoja na kutoa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu, kufanya kazi kwa bidii na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa Umma;

(g) Naomba ufikishe salamu zangu za pongezi kwa viongozi wa mpito wa Chama cha Mawakili wa Serikali kwa jitihada mbalimbali walizoanza kuzifanya kwa ajili ya kutetea maslahi ya Mawakili wa Serikali na wanasheria waliopo katika utumishi wa umma. Pia, nashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iendelee kutumia mfumo wa OAG-MIS kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(h) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itoe kipaumbele kushughulikia changamoto mbalimbali za watumishi ikiwemo kulipa stahili mbalimbali za watumishi kwa wakati kama vile malimbikizo ya mishahara, madai ya likizo, uhamisho, kupandishwa vyeo, kutoa

motisha na kuboresha maslahi ya wafanyakazi ili kutimiza dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuondoa changamoto za watumishi;

(i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iendelee kuwahimiza watumishi kujiendeleza na kupata mafunzo ya muda mrefu au mfupi ili kuongeza ujuzi na maarifa katika maeneo yao ya kazi. Pamoja na jitihada zilizopo za kuendeleza watumishi nashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa mpango endelevu wa kutoa mafunzo kwa watumishi wake kutegemeana na uwezo uliopo wa kifedha: na

(j) Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha wanahamisha ulinzi wa maadili kwa wanafamilia zetu kwa kuwa kwa siku za hivi karibuni kumekua na mijadala mbalimbali ambayo inahusu mmomonyoko wa maadili kwa jamii yetu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza;**

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru tena kwa kunialika kuzindua Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni imani yangu kuwa yote yatakayojadiliwa na kufanyiwa maazimio katika kikao hiki yatasaidia katika kuboresha utendaji wa Wizara na hivyo kuongeza tija na ufanisi.

Ndugu Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza na Wageni waalikwa, baada ya maelezo haya, sasa nachukua fursa hii kutamka kwamba: ***“MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI UMEFUNGULIWA RASMI”***

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.**